

**NB: KIBALI CHA KUSAFIRISHA AU KUAGIZA MAZAO  
YA CHAKULA UTOLEWA BURE HAKUNA GHARAMA  
YOYOTE.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**



***Kwa Mawasiliano:-***

Katibu Mkuu  
Wizara ya Kilimo  
S.L.P. 2182  
**DODOMA**

**Simu: 026-2321407**  
**Email: ps@kilimo.go.tz**

**IDARA YA USALAMA WA CHAKULA  
SEHEMU YA URATIBU MAZAO NA  
TAHADHARI YA AWALI**

## UTANGULIZI

Idara ya Usalama wa Chakula kupitia sehemu ya Uratibu wa Mazao Mashambani na Tahadhari ya Awali ina jukumu kuu la kuratibu uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya chakula katika mikoa yote ya Tanzania Bara katika kipindi chote cha mwaka mzima. Ili kufanikisha hilo Idara ina fanya shughuli zifuatazo:-

- Kufanya tathmini ya Awali ya Uzalishaji wa mazao ya chakula katika mikoa yote mwezi Mei/Juni kila mwaka na kutoa takwimu za Awali za Uzalishaji wa Mazao ya Chakula nchini;
- Kufanya tathmini ya Mwisho ya Uzalishaji wa mazao ya chakula katika mikoa yote mwezi Novemba/Desemba kila mwaka na kutoa takwimu za Mwisho za Uzalishaji wa Mazao ya Chakula nchini
- Kufanya tathmini ya Kina ya Chakula na Lishe katika mikoa na Wilaya zenyne upungufu wa chakula nchini na kutoa makadirio ya idadi ya walioathirika. Zoezi hili hufanyika mara mbili kwa mwaka yaani mwezi Januari/Februari na mwezi Septemba/Oktoba. Wizara hufanya zoezi hili kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu -Idara ya Maafa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI pamoja na wadau wengine wa masuala ya Usalama wa Chakula nchini.
- Kukusanya na kuchambua takwimu za mvua kote nchini. Baadhi ya Vituo hivyo viro chini ya Idara Kuu ya Hali ya Hewa na vigine viro chini ya Wizara ya Kilimo

## UTARATIBU WA KUPATA KIBALI CHA KUSAFIRISHA MAZAO NJE YA NCHI

Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi ndiyo yenyeye mamlaka kisheria ya kutoa vibali vya kusafirisha mazao ya chakula kutoka nje au kwenda nje ya nchi (*Import and Export Permits*).

Kutokana na mamlaka hiyo, ambapo sheria na taratibu uzingatiwa, ufuatao ni utaratibu muhimu ambao mfanyakishara binafsi au kampuni anatakiwa/inatakiwa av/izingatie ili kupatiwa kibali kwa mazao husika.

- Kwanza msafirishaji anatakiwa kuandika barua kwa **Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo** akiomba kibali cha kusafirisha au kuagiza mazao ya chakula.
- Barua iainishe kiasi cha tani kinachotarajiwa kusafirishwa, nchi anakopeleka au anakotoa mazao pamoja na mpaka atakaotumia kupitishia mazao hayo.
- Awe na leseni halali ya biashara (kama anasafirisha nje ya nchi leseni inapatikana Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji).
- Awe na namba ya mlipa kodi (Tin Number).
- Kwa upande wa vyakula vya mifugo maombi yaapitie kwa Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi – Mifugo.
- Taratibu nyingine zote za kusafirisha mazao nje ya nchi (*cheti* cha usajili wa usalama na ufanisi wa chakula na dawa *Tanzania Food and Drug Authority – TFDA phytosanitary Certificate* kutoka Wizara ya Kilimo na Cheti cha Ubora *Certificate of Quality nk*) zitazingatiwa na kufanywa na mamlaka yenyeye dhamana wakati wa kusafirisha.